# UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 11 Januari, 2023




# MIAKA 30 YA KUSIMAMIA KURATIBU NA KUENDESHA CHAGUZI

IFAHAMU TUME

# MZUNGUKO WA UCHAGUZI

**Kukosa sifa za kuandikishwa kuwa Mpiga Kura**

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 pamoja na Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mtu hatakuwa na sifa za

kuandikishwa kama Mpiga Kura iwapo:-
(i) Ni raia wa nchi nyingine
(ii) Ana utii kwa nchi nyingine (Allegiance to another country)
(iii) Imethibitishwa kuwa hana akili timamu;
(iv) Amehukumiwa adhabu ya kifo na Mahakama;
(v) Anatumikia adhabu ya kifungo kinachozidi miezi sita gerezani;
(vi) Amezuiliwa kujiandikisha kuwa Mpiga Kura na Sheria za Uchaguzi ama Sheria nyingine kwa makosa yanayohusiana na uchaguzi; au
(vii) Hatakuwa ametimiza umri wa kupiga kura, ifikapo siku ya uchaguzi.



# Miaka 30 ya kusimamia, kuratibu na kuendesha chaguzi

***Na Mwandishi wetu***

Miaka 30 imepita sasa tangu ilipoundwa rasmi Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) mnamo tarehe 13 Januari, 1993. Ni miongo mitatu ya kuendesha chaguzi zenye weledi na zinazozingatia Katiba, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali inayotolewa na Tume.

Utashi wa kisiasa ndio haswa uliopelekea kuanzishwa kwa Tume ambapo Februari 07, 1991 aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Alhaj Ali Hassan Mwinyi aliteua Tume ya

watu 40 iliyoongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Jaji Francis Nyalali.

Tume hiyo ilipewa kazi ya kukusanya maoni ya wananchi juu ya kuendelea au kutoendelea na mfumo wa chama kimoja cha siasa.

Baada ya kukusanya maoni, asilimia 80 ya Watanzania walitaka kiwepo chama kimoja na asilimia 20 walitaka vyama vingi.

Hata hivyo, licha ya maoni ya wananchi wengi katika ripoti ya Tume ya Nyalali kupendekeza mfumo wa chama kimoja serikali iliona ni busara nchi ikaingia kwenye mfumo wa vyama vingi ili kuimarisha demokrasia.

Aidha, ripoti ya Tume ya Jaji Nyalali ilipendekeza iundwe upya Tume ya Uchaguzi itakayosimamia chaguzi chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Mapendekezo hayo ndiyo yaliyosababisha kuundwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Kutokana na mapendekezo hayo Serikali ilifanya marekebisho ya Katiba na Sheria mbalimbali za uchaguzi ili kuendana na mfumo wa vyama vingi.

Sura ya 3 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ilirekebishwa na kufanya Tanzania kuwa Taifa linalofuata mfumo wa Vyama vingi vya Siasa.

Aidha, Sheria ya Vyama vya Siasa, (Na. 5 ya 1992) ilirekebishwa ili kuruhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, (Na.1 ya 1985), Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa (Na. 4 ya 1979) na sheria zinazoendana pia zilirekebishwa ili kuondokana na matakwa ya chama kimoja na kuruhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Hivyo, mapendekezo ya Tume ya Jaji Nyalali yalisababisha kuundwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Januari 13, 1993 na Rais Mwinyi aliwateua Wajumbe wa Tume, Januari 14, 1993.

Tume iliundwa chini ya Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Pamoja na majukumu mengine, Tume imepewa jukumu la Kusimamia, Kuratibu na Kuendesha Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Chaguzi za Madiwani wa Tanzania Bara.

Aidha, Ibara ya 74(7) ya Katiba inatamka kwamba Tume ni idara huru inayojitegemea.

Tangu ianzishwe, Tume imeendesha Chaguzi kuu sita (6) za Rais, Wabunge, na Madiwani. Chaguzi hizo zilifanyika mwaka 1995, 2000, 2005, 2010, 2015 na 2020. Tume pia iliratibu, kusimamia na kuendesha Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994.




# Wenye ulemavu wafurahia Tume kuwajali

***Na Mwandishi wetu***

Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) kimeeleza kufurahishwa na kuwepo huduma maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwenye banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa maonesho ya Wiki ya Sheria Kitaifa yaliyofanyika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Akizungumza baada ya kutembelea banda la Tume kwenye maonesho hayo, Katibu wa CHAVITA Mkoa wa Dodoma, Bi. Amina Issah, alisema amefurahishwa kuona majalada ya nukta nundu na wakalimani wa lugha ya alama kwenye banda la Tume, jambo linalorahisisha mawasiliano kwa watu wote.


"Mara nyingi tumekuwa tukisisitiza kuwepo kwa karatasi zenye maandishi ya nukta nundu na

wakalimani wa viziwi. Leo tumekuta karatasi za watu wasioona zipo na wakalimani wa viziwi wapo, tumefurahishwa sana na inarahisisha mawasiliano na kudumisha ushirikiano" alisema Amina.

Amina aliipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kutoa huduma hizo na kuongeza kwamba kwa kufanya hivyo inakuwa mfano wa kuigwa kwa taasisi nyingine kutoa kipaumbele katika kuwahudimia watu wenye ulamavu.

"Ushauri wangu kwa taasisi nyingine wafuate mfano wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Ni taasisi pekee iliyoonesha mfano mzuri kwa vitendo, watumishi wamejifunza lugha ya alama jambo ambalo linatutia moyo," aliongeza Amina.

Maonesho ya Wiki ya Sheria yalifanyika kuanzia tarehe 24 Januari hadi tarehe 1 Februari 2023 ambapo Taasisi mbalimbali za Serikali na wadau wa sheria nchini walishiriki.



# Tume yashiriki maonesho mapinduzi matukufu ya Zanzibar




***Na Mwandishi wetu***

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeshiriki maonesho ya Sherehe za Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yaliyofanyika kwenye viwanja vya Maisara, Unguja, Tanzania Zanzibar.

Maonesho hayo yamefanyika kuanzia tarehe 1 hadi 12 Januari, 2023, ambapo Tume ilishiriki kwa kutoa Elimu ya Mpiga Kura kwa wananchi waliotembelea maonesho hayo.

Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji Rufaa

(Mst), Mbarouk Salim Mbarouk alitembelea banda la Tume na kufurahishwa na ushiriki wa Tume kwani uliwawezesha wapiga kura wa Zanzibar kupata elimu na kutambua majukumu ya Tume.

Kwa upande wake Mkurugezi wa Uchaguzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Bw. Thabit Idarus Faina ambaye naye alitembelea banda la Tume na kuzungumza na watumishi wa NEC waliokuwa kwenye banda hilo na kueleza kuridhishwa na huduma iliyokuwa inatolewa.

Watumishi mbalimbali wa Tume wakiongozwa na Mkurugenzi Ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar, Bw. Adam Mkina waliwahudumia wananchi waliofika kwenye banda la Tume kwa kupokea na kujibu maswali yao.

Kaulimbiu ya Sherehe za Miaka 59 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ilikuwa ni "Mapinduzi Yetu Ndio Amani Yetu, Tuyalinde kwa Maendeleo Yetu".





# Pinda aipongeza Tume utunzaji wa mazingira

***Na Mwandishi wetu***

Waziri Mkuu Mstaafu Mh. Mizengo Pinda ameipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kutunza mazingira ikiwa ni pamoja na miti aliyoshiriki kuipanda Desemba 2,2021 kwenye eneo la Ofisi za Tume Njedengwa, jijini Dodoma.

Pinda aliyasema hayo hivi karibuni wakati akikagua miti hiyo na kutoa maelekezo ya namna bora zaidi ya kuikinga isiharibiwe na upepo.

Waziri Mkuu huyo Mstaafu aliyekuwa ameongozana na Mwenyekiti wa Tume, Mh. Jaji wa Rufaa Jacobs Mwambegele na Mkurugenzi wa uchaguzi wa Tume, Dkt. Wilson Mahera Charles alishauri pia eneo lililopandwa nyasi za ukoka kuwekwa mbolea ya maji ili zistawi na kupendeza



# Watumishi Tume wanufaika na program za mafunzo India

***Na Mwandishi wetu***

Serikali ya India kupitia Programu yake ya Indian Technical and Economic Cooperation (ITEC) imetoa nafasi za kuwajengea uwezo watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika masuala mbalimbali ya kiutendaji kazi.

Katika kipindi cha mwezi Disemba 2022 na Januari, 2023, Watumishi 9 wamepata nafasi ya kuhudhuria mafunzo katika taasisi ya Kimataifa ya Demokrasia na Usimamizi wa Uchaguzi India (India International Institute of Democracy and Election Management-**IIIDEM**).

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mafunzo, Bw. Michael Kiria ambaye ni mnufaika amesema mafunzo hayo yamemuongezea uelewa mkubwa katika utoaji wa Elimu ya Mpigakura.

Utaoji wa elimu ya mpiga kura ni moja ya jukumu la Tume lililoainishwa chini ya Kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Bw. Kiria anaamini kwamba ujuzi alioupata kwenye mafunzo hayo utamuongezea uwezo wa kutoa elimu ya mpiga kura na kusababisha kufikiwa kwa malengo ya Tume ya kuongeza idadi ya wananchi wanaoshiriki katika chaguzi mbalimbali zinazofanyika nchini.

Ameushukuru Uongozi wa Tume kwa kumpa nafasi ya ushiriki na Serikali ya India kwa kufanikisha mafunzo hayo.

“Katika nchi yetu kumekuwa na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii hasa wakati wa uchaguzi, hivyo mafunzo haya yameniwezesha kujua ni kwa namna gani naweza kushiriki katika utoaji wa habari zilizo na uhakika kwa umma kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii” alisema Bw. Mathew Kwembe ambaye ni mnufaika wa mafunzo hayo.

Bi. Fina Kidunda ambaye naye alishiriki mafunzo amesema mafunzo haya yamekuwa na mchango mkubwa hasa katika taaluma yake na utendaji kazi wa Tume hivyo ameiomba serikali ya India kuendelea kutoa mafunzo haya kwa watumishi wa idara mbalimbali za serikali ili kuongeza tija katika utendaji kazi wa kila siku.

Serikali ya India kupitia Wizara ya mambo ya Nje inasimamia program ijulikanayo kama Indian Technical and Economic Cooperation (ITEC) ambayo ilianzishwa mwaka 1964 kwa ajili ya kujenga ushirikiano katika masuala ya kiufundi na kiuchumi.

Ilianzishwa ikiwa na nchi mbili washiriki, sasa ina nchi washiriki 158 huku ikisimamia utoaji wa kozi mbalimbali katika vyuo vilivyopo nchini India.

Mojawapo ya vyuo ambavyo vipo kwenye mpango huo ni IIIDEM kilichoanzishwa na Tume ya Uchaguzi ya India (ECI) kwa lengo la kusaidia usimamizi bora wa uchaguzi nchini India, kukuza ushiriki wa watu, kuchangia kuendeleza taasisi katika uimara kwenye demokrasia na kuunga mkono juhudi za ECI katika kutekeleza majukumu na kazi zake.



# Warsha ya Watumishi Tume kuhusu magonjwa, rushwa na mafao

***Na Mwandishi wetu***

Watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wamepatiwa mafunzo maalum ya kujilinda na maambukizi ya Ukimwi, magonjwa yasiyoambukiza, mapambano dhidi ya rushwa, utunzaji wa nyaraka na mafao baada ya kustaafu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Bw. Leonard Tumua amesema utoaji wa mafunzo hayo ni utekelezaji wa Mwongozo wa Ukimwi na magonjwa yasiyoambukiza katika utumishi wa Umma uliotolewa mwaka 2014 na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

"Mwongozo huo umetoa maelekezo ya kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu ukimwi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa watumishi kwa kuwa magonjwa haya yamesababisha kupotea kwa nguvu kazi, mahudhurio hafifu mahali pa kazi, kupungua kwa ufanisi na kuongeza mzigo wa kazi kwa watumishi wengine,"alisema Tumua.

Aidha, mada nne tofauti zilitolewa katika mafunzo hayo zilizohusu Ukimwi Mahala pa Kazi, Rushwa, Utunzaji wa Nyaraka na Mafao ya Kustaafu.

Bw. Tumua aliwataka watumishi kuzingatia mafunzo hayo hasa ya Ukimwi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwani Serikali kama mwajiri imekuwa na matumizi makubwa ya rasilimali fedha yanayosababishwa na magonjwa hayo.

Akizungumza kuhusu rushwa, Bw. Tumua alisema mafunzo hayo yanafanyika ikiwa ni mwendelezo wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Awamu ya Tatu. Mafunzo hayo yalihusu masuala ya uadilifu na mapambano dhidi ya rushwa ili kuimarisha Utawala Bora.

"Kumekuwa na changamoto nyingi katika nyakati hizi kuhusu utumiaji na utunzaji wa nyaraka za Serikali. Hivyo, Tume imeona ni vyema kukumbushana kuhusu taratibu za matumizi na utunzaji wa nyaraka za Serikali" alisema.

Kuhusu mafunzo ya mafao ya kustaafu, Bw. Tumua alisema Tume iliandaa mafunzo hayo ikiwa ni sehemu ya maandalizi kwa ajili ya watumishi wanaokaribia kustaafu na watumishi wote kwa ujumla kwa kuwa watumishi wote ni wastaafu watarajiwa.





# Wanamichezo NEC watakiwa kujitoa zaidi

***Na Mwandishi wetu***

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Dkt.Wilson Mahera Charles amewataka watumishi wanamichezo wa Tume kuendelea kujitoa zaidi ili waweze kuleta vikombe na medali nyingi za ushindi katika mashindano yajayo.

Wito huo ameutoa hivi karibuni wakati akikabidhiwa ripoti ya ushiriki wa michezo ya SHIMIWI 2022 kwa Timu ya NEC Sports sambamba na Kikombe cha ushindi wa pili wa karata kwa wanawake katika ukumbi wa kutangazia matokeo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi uliopo Njedengwa, jijini Dodoma.

Dkt. Mahera amesema ana imani kubwa na wanamichezo hao hivyo

amewataka kuongeza juhudi zaidi hasa katika kufanya mazoezi ili waweze kushiriki na kushinda katika mashindano yajayo.

Awali akizungumza wakati akiwasilisha ripoti ya ushiriki wa michezo hiyo ya SHIMIWI kwa mwaka 2022, Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya NEC (NEC Sports Club), Bw. Juvenille Kaiza amemshukuru Dkt. Mahera kwa kuziwezesha timu za NEC Sports kushiriki michezo hiyo.

Bw. Kaiza aliahidi kuendelea kufanya vizuri katika mashindano yajayo na kushinda vikombe zaidi.

Timu ya NEC Sports ilifanikiwa kushinda kikombe kwa kuwa mshindi wa pili katika mchezo wa Karata wanawake huku timu ya kamba wanaume na wanawake zikiishia katika hatua ya makundi kwenye michezo ya SHIMIWI 2022 iliyofanyika jijini Tanga.






Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV